



*SUN Civil Society Alliance in Tanzania*

**PONGEZA KWA MH. SAMIA SULUHU HASSAN RAIS WA JAMUHURI YA  
MUUNGANO WA TANZANIA KWA KUENDELEA KUSIMAMIA MKATABA WA LISHE  
NA WAKUU WA MIKOA**

Jukwaa la Lishe Tanzania (PANITA); linapenda kuchukua fursa hii kumpongeza kwa dhati Mh. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Kusimamia vyema suala la kutokomeza UDUMAVU (Stunting) na matatizo mengine yatokanayo na lishe duni nchini. Aidha, nia yake ya dhati katika kuhakikisha utapiamlo unakuwa historia nchini umedhihirishwa na majibu aliyojatoa katika mukutano wake na Wahariri wa vyombo mbalimbali vya habari mnamo tarehe 28/06/2021 Ikulu Dar es salaam. Aidha, kupitia maelezo hayo Mh.Rais alionyesha umahiri na uelewa mkubwa juu ya tatizo la utapiamlo nchini na jinsi linavyochangia katika matatizo ya afya ya mama na mtoto wakati anajibu swali la Mhariri Mkuu wa Vyombo vya Habari vya Clouds, Joyce Shebe. Mhe. Rais alisema, nanukuu:

*"Nilipokuwa Makamu wa Rais, Nilijipa kazi ya kujishughulisha na sekta ya Afya, na nikashughulika na afya ya Mama na mtoto. Kwenye afya ya mama na mtoto tulijielekeza sana katika ujengaji wa vituo vya afya na zahanati ili kusogeza huduma za afya karibu zaidi na wananchi na kwa kiasi fulani tumeweza. Lakini pia nikajiingiza kwenye swala hili la lishe, nikaingia mikataba na Wakuu wa mikoa, na kila Mkuu wa mkoa nilimtaka asimamie lishe kwenye mkoa wake. Mbaya zaidi*

*ilikuwa kwenye ile mikoa ambayo tunaiita ni mikoa ya vyakula, mikoa ya katikati hapa Morogoro, Iringa Mbeya na kanda za juu kusini ndio mikoa amabayo inalima vyakula vyote, lakini ndio mikoa yenyе kiasi kikubwa cha utapiamlo na udumavu, mpaka Kigoma kule juu. Kwa hiyo kwa kuingia mikataba na wakuu wa Mikoa, nilikuwa nawabana na wameweza kupunguza hali hii kwa kiasi kikubwa, kwa hiyo sasa nitaifanya hiyo kazi nikiwa katika hiki kitи cha Urais ambapo najua wakuu wa mikoa watajituma zaidi ili kuondosha tatizo hili.”*

Sambamba na hilo aliahidi kuendelea kusimamia kwa karibu mkataba wa lishe baina yake na Wakuu wa mikoa ambao unaratibiwa kupitia TAMISEMI. Mkataba huu ulisainiwa wakati Mh. Samia Suluhu Hassan akiwa Makamu wa Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania mwezi Disemba 2017. Tangu kusainiwa kwa mkataba huu tumeshuhudia kuongezeka kwa uwajibikaji katika ngazi ya Mkoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika usimamiaji na utekelezaji wa afua za lishe katika maeneo yao. Sambamba na hilo, pia kuna ongezeko la bajeti katika utengaji na utoaji wa fedha za shughuli za lishe kutoka vyanzo vya ndani vya halmashauri.

Jukwaa la lishe Tanzania (PANITA) tumefarijika sana kwa kauli hii ya Mh. Rais kwani mnamo tarehe 20/07/2016 tulimualika Mh. Samia Suluhu Hassan katika uzinduzi wa ripoti ya lishe ya Dunia 2016; na katika hadhara ile, kupitia Mh. Dunstan Kitandula (Mbunge wa Mkinga) ambaye aliungana nasi kwa nafasi ya Mwenyekiti wa Kikundi cha Wabunge Vinara wa Lishe, Usalama wa Chakula na Haki za Watoto Bungeni, tulimuomba Mh. Samia Suluhu kuwa Kinara wa Lishe wa Taifa, jukumu ambalo alilikubali bila kusita na sasa tunaona matunda yake. Tunakushukuru sana Mh. Rais Samia Suluhu kwa kuwa mfano bora wa Kiongozi wa kisiasa ambavyo wanaweza kushughulikia masuala ya lishe katika maeneo wanayoyaongoza. Kwa

muktadha huu tunaamani tutafika pahala, tatizo la Utapiamlo litakuwa historia Tanzania. Tunakushukuru sana Mh. Rais kwa kuendelea kulisimamia jambo hili kikamilifu; na sisi kama PANITA tunaendelea kushiriki katika vita hii ya kutokomeza utapiamlo nchini kwa nguvu na ari kubwa. Kwa mara nyingine tena, tunasema ahsante sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**Imetolewa na: Mkurugenzi Mtendaji**

*Partnership for Nutrition in Tanzania (PANITA)*

**Maelezo kwa Mhariri**

Jukwaa la Lishe Tanzania (PANITA) ni mtandao unaouunganisha Asasi za Kiraia zinazojishughulisha na masuala ya Lishe. Lengo kubwa la PANITA tangu kuanzishwa kwake mwaka 2010 ni kuboresha hali ya lishe katika nchi yetu kwa kushirikiana na serikali pamoja na wadau mbalimbali ikiwamo wafadhili, wanahabari, wabunge, watunga sera pamoja na jamii kwa ujumla. PANITA ina Asasi wanachama wapatao 346 waliopo mikoa yote Tanzania.

Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kupitia:

*Off Rose Garden Road, 6 Rwehabura Road,*

*Plot No. 305A, Mikocheni A,*

*P.O. Box 32095, Dar es Salaam, Tanzania.*

*Tel: +255 222 701 753*

*Email: info@panita.or.tz*

*www.panita.or.tz*